**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025]*

---

Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

**05 Mei, 2026**

## IKISIRI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Bunge,2025. Madhumuni yake ni kuliwezesha Bunge kuijadili na kupitisha mapendekezo ya Kamati kadiri yalivyo au kwa kuyarekebisha.

Taarifa imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya Jumla na sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na kuonesha uchambuzi unaotokana na shughuli za Kamati. Sehemu ya tatu ina bainisha mtazamo na maoni ya Kamati kuhusu, Sekta ya Maji. Uchambuzi umebainisha utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya bajeti kwa Mwaka 2025/2026. Utekelezaji huo unaweza ukaonyeshwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni utekelezaji unaoridhisha na kundi la pili ni utekelezaji wa maazimio ulio katika hatua isiyoridhisha

Vile vile, uchambuzi umeonesha mafanikio na changamoto mbalimbali kwa Sekta ya Maji. Changamoto zilizobainishwa ni ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza Miradi Mikubwa ya Kimkakati, Madai ya Wakandarasi, Washauri Elekezi na Wazabuni, Uchakavu wa Mabomba na Upotevu wa Maji Njiani Kabla ya Kufika kwa Walengwa, Mabadiliko ya Tabianchi na malimbikizo ya Madeni ya Ankara za matumizi ya Maji.

Changamoto nyingine ni Uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji na gharama kubwa za uendeshaji na Mabadiliko ya Tabia nchi.

Kutokana na changamoto hizo Taarifa imebeba mapendekezo katika maeneo Nane yafuatayo: -

(i) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ya maji;
(ii) Malimbikizo ya deni la Ankara za maji;
(iii) Madai ya Wakandarasi na Washauri Elekezi kwenye miradi ya maji nchini;
(iv) Uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji;
(v) Uelewa mdogo wa Jamii kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji;
(vi) Upotevu wa maji yanayopotea njiani kutokana na sababu mbalimbali;
(vii) Mabadiliko ya tabianchi; na
(viii) Kasi ndogo ya Kufunga dira za maji za malipo kabla ya matumizi (*prepaid water meters*).

# YALIYOMO

*Ukurasa*


IKISIRI i

**YALIYOMO……………………………………………………………………………………ii**

**ORODHA YA VIFUPISHO NA MAANA…………………………………………………………iii**

**ORODHA YA VIELELEZO…………………………………………………………………………iv**

**SEHEMU YA KWANZA........................................................................................................ 1**

1.0 UTANGULIZI……………………………………………………………………………1

1.1 Maelezo ya Awali ……………………………………………………………………1

1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati.................................................................................2

**SEHEMU YA PILI………………………………………………………………………………4**

**2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI ……………………………………………………………4**

2.1 Maelezo ya Jumla……………………………………………………………………4

2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ...........................................................................................................5

2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 .............................................................................................................5

2.2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo...................................................8

2.2.3 Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Maji – Kidunda-Morogoro .................................8

2.2.4 Mradi wa Usambazaji Maji Dambia – Haydom Wilaya ya Mbulu....................10

2.2.5 Mradi wa Nanja Wilaya ya Monduli. ..................................................................11

2.2.6 Mradi wa Maji Same – Mwanga (SAMWASA) ....................................................12

2.2.7 Mradi wa Ujenzi wa kusambaza Maji Mkinga - Horohoro................................14

2.2.8 Makusanyo ya Maduhuli.........................................................................................15

2.2.9 Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida..................................17

2.2.10 Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo....................................................19

2.2.11 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ...........................................................................22

**SEHEMU YA TATU……………………………………………………………………… ……26**

**3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027...........................………26**

3.1 Uchambuzi wa Malengo na Vipaumbele .........................................................….26

3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027......................................... ..27

3.2.1 Makadirio ya Maduhuli Yatakayokusanywa……………………………27

3.2.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti FUNGU 49…………………………29

3.2.3 Mchanganuo wa Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 ……………………30

3.2.4 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ……………………31

3.2.5 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti ya Serikali ……………………………………………………………………………………33

**3.3 MAONI NA USHAURI WA KAMATI……………………………………………………35**

3.3.1 Maoni ya Kamati.........................................................................................................35

3.3.2 Ushauri wa Kamati .....................................................................................................37

3.3.3 Hitimisho .....................................................................................................................43

## ORODHA YA VIFUPISHO NA MAANA

| | |
|---|---|
| **PPP** | Public Private Partnership |
| **CCM** | Chama cha Mapinduzi |
| **PE** | Personal Emolument |
| **RUWASA** | Rural Water Supply and Sanitation Agency |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals |
| **TAMISEMI** | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **O.C.** | Other Charges |
| **TANGA – UWASA** | Tanga Urban Water Supply and Sanitation Authority |
| **TAM** | Tathmini ya Athari kwa Mazingira |
| **CBWSOs** | Community Based Water Suppply Organization |
| **KVA** | Kilo Volt Amperes |
| **VAT** | Vat Added Tax |
| **SAMWASA** | The Same - Mwanga Water and Sanitation Authority |
| **NWF** | National Water Fund Tanzania |

## ORODHA YA VIELELEZO


**Kielelezo Na. 1** Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Kielelezo Na. 2** Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na Kupokelewa hadi Februari, 2026

**Kielelezo Na. 3** Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo hadi Februari, 2026

**Kielelezo Na. 4** Ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Kielelezo Na. 5** Ulinganisho wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Kielelezo Na. 6** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali 2026/2027

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Mkutano wa kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mara ya kwanza katika Bunge hili la 13.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu (3): -

(i) Sehemu ya 1 inahusu utangulizi ambayo inahusisha msingi na muundo wa taarifa;

(ii) Sehemu ya 2 ni kuhusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iii) Sehemu ya 3 ni Maoni, Ushauri, Mapendekezo ya Kamati kwa Serikali na Hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6(6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji **(Fungu 49)**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 ambayo, imeweka masharti yanayoitaka Kamati kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 120 (2) inazitaka Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Maji na Mazingira kuchambua Taarifa za Bajeti kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 14 -18 Machi, 2026, Kamati ilitembelea Miradi 5 ya Maendeleo iliyotengewa fedha na Serikali chini ya Wizara ya Maji. Pia ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maji **Fungu 49**

kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inafafanua Uchambuzi katika maeneo yafuatayo: **-**

(a) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na;

(b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** njia iliyotumika kufanya uchambuzi inajumuisha kulinganisha hali ilivyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Njia ya ukokotoaji wa asilimia imetumika kubaini hatua inayofikiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha na kujiridhisha na uwezekano wa mipango inayolengwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilijikita katika maeneo Makuu Matano yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Matokeo ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Hali ya Makusanyo ya Maduhuli;

(iv) Hali ya Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 na;

(v) Utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa ufuatiliaji na uamuzi wa Kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kamati ilitoa Ushauri katika maeneo saba (7). Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Ushauri wa Kamati umezingatiwa

japo sio kwa asilimia mia moja, kwa sababu maoni yote yaliyotolewa yapo kwenye hatua za utekelezaji kama ifuatavyo: -

a) Ushauri kuhusu kuhamasisha Mamlaka ya Maji Tanga kufanya vizuri kwenye Hati Fungani ya Kijani *(Green Bond)*;

   **Mheshimiwa Spika,** Kamati imetaarifiwa kuwa, Serikali, Kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji, imeendelea kuisimamia na kuihamasisha Mamlaka ya maji Tanga kufanya vizuri katika matumizi ya fedha za Hati Fungani, na kulipa kwa wakati wawekezaji ili kuvutia mamlaka nyingine kuiga. Ni dhamira ya Serikali kuendelea kutumia mfumo wa Hati Fungani za Kijani (Green Bond), kama mbinu bunifu ya kupata rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya maji na usafi wa mazingira. Aidha, Kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji, Wizara tayari imetangaza zabuni ya kumpata Mtaalam Mshauri ambaye kwa sasa anaendelea na mchakato wa kuwezesha mamlaka nyingine za maji kutumia mfumo huo.

b) Ushauri kuhusu Taasisi tisa (9) za Umma zinazodaiwa ankara za matumizi ya maji kiasi cha **Shilingi 61,421,854,197.70.** kulipa madeni hayo kabla ya tarehe 30/06/2025.

   **Mheshimiwa Spika,** Kamati imepokea taarifa kuwa, Serikali kupitia Mamlaka za Maji, imeendelea kuzifuatilia taasisi husika ili kuhakikisha zinalipa madeni

yao kwa wakati. Vilevile, Mamlaka za Maji zitaendelea kufunga dira za maji za malipo kabla ya matumizi (*prepaid meters),* katika taasisi za umma. Aidha, hadi Mwezi Februari 2026, jumla ya taasisi za umma **52** zimefungiwa dira hizo.

c) Kuhusu Serikali kulipa madai ya Wakandarasi kiasi cha **Shilingi 534,725,071,524.31.** Kabla ya tarehe 30 Juni, 2025 ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kwa kutopatikana kwa fedha hizo;

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa jambo hili ni kwamba, Serikali imeendelea kulipa madai ya Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo, hadi Februari, 2026 jumla ya Shilingi **bilioni 261.7.** Sawa na **asilimia 49**. zimelipwa kwa Wakandarasi, Washauri elekezi na Wazabuni wa huduma nyinginezo.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza ushauri huo. Aidha inasisitiza kuendelea kulipa madeni hayo ili miradi ikamilike kwa wakati.**

d) Kuhusu kukabiliana na upungufu wa lita **milioni 70.4** za maji kwa siku katika Jiji la Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepokea taarifa kuwa, Utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa mtandao wa maji safi Nzuguni, unaogharimu **shilingi bilioni 5.51.** Unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026.

Mradi huu ukikamilika utaongeza upatikanaji wa lita za maji **Milioni 15** kwa siku.

**Mheshimiwa Spika, Ni rai ya Kamati kwamba, Serikali iendelee kutekeleza miradi ya maji kwa kubuni na kusanifu vyanzo vingine vya maji ili kukidhi mahitaji ya maji katika Mji wa Dodoma.**

### 2.2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii katika Mkoa wa Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Morogoro. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu matokeo ya Ukaguzi wa Miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.3 Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Maji – Kidunda-Morogoro

**Mheshimiwa Spika**,  ujenzi wa Bwawa la kuhifadhia maji Kidunda utanufaisha katika Mikoa mitatu ambayo ni Dar es salaam, Pwani na Morogoro. Ujenzi huo ulianza tarehe 18 Juni, 2023 na  unatarajiwa kukamilika tarehe 17 Juni, 2026, kwa gharama  ya **Shilingi. 329,466,814,886.00.** Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 utekelezaji wa mradi  huu ulikuwa umefikia **asilimia 47.** ya lengo. Jumla ya fedha zilizolipwa ni **Shilingi bilioni 128.70.** Hadi kufikia Februari , 2026**.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ukikamilika utaleta uhakika wa upatikanaji wa maji, kwa ajili ya matumizi ya majumbani na shughuli za kiuchumi, kama vile, Kilimo cha umwagiliaji. Aidha, mradi huu ukikamilika unatarajiwa kuwanufaisha wananchi wapatao **11,387,700.**

**Mheshimiwa Spika,** changamoto za mradi ni kama zifuatazo -:

(i) Kuchelewa kutolewa kwa fedha za miradi kwa wakati;

(ii) Miundombinu mibovu ya barabara inayokwenda eneo la mradi;

(iii) Uharibifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji, unaotokana na shughuli za kibinadamu, ikiwemo ufugaji holela, kilimo na ujenzi wa makazi katika vyanzo vya maji; na

(iv) Mradi huu unakabiliwa na suala la kutokupatikana kwa Msamaha wa kodi kwa wakati. (custom/*import duty)*.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali, kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu mkubwa. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kuendelea kutoa fedha kikamilifu na kwa wakati ili kukamilisha Mradi.**

### 2.2.4 Mradi wa Usambazaji Maji Dambia – Haydom Wilaya ya Mbulu

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Mbulu kata ya Bashay Mkoani Manyara. Mradi ulianza kutekelezwa Mwezi Februari, 2024 na unategemewa kukamilika Novemba 2027. Mradi huu utakapokamilika utaweza kuhudumia vijiji 21 na kunufaisha jumla ya wananchi wapatao **133,737.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi una gharama ya **Shilingi 41,213,744,936.44**. Hadi kufikia mwezi Machi , 2026, Mkandarasi tayari ameshalipwa kiasi cha **Shilingi 10,197,420,827.25.** Na kuwezesha utekelezaji wa **asilimia 44.5.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi umetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa fensi eneo la kusukuma maji lilipojengwa tanki kuu la lita **2,000,000** katika kijiji cha Harsha;
(ii) Ujenzi wa tenki la juu lenye ujazo wa lita **75,000** katika kijiji cha Yaendakati;
(iii) Ununzi wa Gari aina ya *Toyota Land Cluiser Double Cabin*; na
(iv) Ujenzi wa Tenki lenye lita **500,000** eneo la chanzo cha maji Dambia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini usambazaji mdogo wa maji kutoka kwenye tanki kuu kwenda kwenye vijiji vya

jirani kutokana na upungufu wa fedha wa **Shilingi Milioni 150**.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa Rai kwa Serikali, kuhakikisha Mkandarasi huyo analipwa kiasi cha fedha kilichobaki ili aweze kukamilisha usambazaji wa maji kwa wakati.**

### 2.2.5 Mradi wa Nanja Wilaya ya Monduli.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulianzishwa baada ya kuwepo kwa changamoto ya vyanzo vya maji. Vijiji kumi na tatu (13) kijiji cha Monduli. Changamoto hii ilipelekea kuibuliwa kwa mradi huu wa kutoa maji kwenye Skimu ya Arusha ambapo mahitaji yake ni lita **6,048,000,** kwa siku kutoka katika tanki kubwa la lita **10,000,000,** la Ngaramtoni Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa kwa muda wa Miaka 3 na nusu, kuanzia April, 2024 hadi Disemba, 2026 kwa gharama ya **Shilingi 20,321,980,809.** Mradi huo umefikia **Asilimia 11** tu ya Lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka 2025/2026, Mradi huu uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,300,000,000.00.** Hadi kufikia Februari, 2026 Mradi ulikuwa umeshapokea kiasi hicho cha fedha kama kilivyoidhinishiwa na Bunge sawa na **asilimia 100.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati Ilipotembelea mradi huu tarehe 14 Machi, 2026 ilibaini kuwa, Mradi huu utakapokamilika utahudumia wananchi **57,791** pamoja na mifugo **161,080** katika vijiji **13**. Aidha, baadhi ya vijiji hivyo ni pamoja na Meserani juu, Meserani Bwawani, Arkatani, Lashaine, Arkaria, Mtimmoja, Nanja, Lepruko, Losimingori, En'garoji, Naalarami, Engorika, Lengiloriti na mji mdogo wa Monduli pamoja na Zahanati **13,** shule za msingi **14**, na shule za Sekondari **3**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto ya kutengewa fedha kidogo, jambo linaloweza kuchelewesha kukamilika kwa wakati;

**Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza Serikali, kuongeza kasi katika kutekeleza mradi huu, kwani ni Mradi muhimu katika kuwasaidia Wakazi wa maeneo ya Monduli yenye adha kubwa ya maji safi na Salama.**

### 2.2.6 Mradi wa Maji Same – Mwanga (SAMWASA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ilipata fursa ya kutembelea na kukagua mradi huu Tarehe 14 Machi, 2026. Mradi huu utahudumia wananchi wanaoishi katika vijiji **38** vya Mradi yaani, vijiji **17** Wilaya ya Mwanga, 1**6** Wilaya ya Same na **5** katika Wilaya ya Korogwe. Mradi ulikadiliwa kutumia kiasi cha **Shilingi 406,103,960,070.35.** Hadi kufikia Februari, 2026

**Shilingi Millioni 300.** Zilikuwa zimeshatumika kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kata **8** zilizopitiwa na Mtandao wa Usambazaji Maji, ambapo, wakazi wapatao **57,105** sawa na **asilimia 95,** waishio kata za Mjini (Mwanga, Same, Stesheni na Kisima) wanapata huduma ya majisafi na salama na **asilimia 80,** ya wakazi waishio kata za vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo Kamati ilibaini mafanikio yafuatayo -;

(i) Kukamilika kwa mradi awamu ya kwanza umeongeza upatikanaji wa huduma hiyo kutoka wastani wa **asilimia 45** hadi **95**;

(ii) Kuendeleza mtandao wa mabomba ya maji (km18) kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa wananchi;

(iii) Mamlaka imefunga visima viwili kijiji cha Same na Mwanga;

(iv) Upatikanaji wa ajira katika kusimamia huduma za maji kupitia CBWOs;

(v) Ujenzi wa Matanki 7 katika maeneo mbalimbali yenye jumla ya ujazo wa Lita **32,500,000**; na

(vi) Ulazaji wa bomba za kusafirisha maji safi yaliyotibiwa hadi kwenye kituo cha kusukuma maji Kisangara na ujenzi wa Kidakio cha maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

(i) Kuongezeka kwa gharama kubwa za uendeshaji, hasa matumizi ya umeme;
(ii) Uhaba wa vitendea kazi vya kisasa hasa katika eneo la usimamizi wa maji; na
(iii) Wananchi kutolipa bili za maji kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali, kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu, sambamba na maandalizi ya awamu ya pili ya mradi.**

### 2.2.7 Mradi wa Ujenzi wa kusambaza Maji Mkinga - Horohoro

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu, unatekelezwa katika Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga kwa fedha kutoka Serikali Kuu na mfuko wa Taifa wa Maji (*NWF)*. Mradi Ulianza kutekelezwa Novemba, 2022 na unategemewa kukamilika Julai, 2026. Awamu ya kwanza ya mradi inagharimu **Shilingi 35,472,451,838.59.** Aidha, kiasi cha maji kinachochukuliwa kutoka kwenye Skimu ya Tanga ni lita **8,294,400,** kwa siku na kuwahudumia wakazi wapatao **42,526** katika vijiji **27**.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2026 mradi umepokea kiasi cha **Shilingi 11,320,867,775.79.** Sawa na **asilimia 32** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea mradi huu ilijulishwa kuwa utekelezaji umefikia **asilimia 65** na kufanikisha kazi zifuatazo: -

(i) Usanifu wa miundombinu na mtandao wa bomba kuu kutoka chanzo cha Maji Mowe hadi Horohoro Mpakani, na mabomba ya usambazaji yenye urefu wa kilomita **196.1.** Utekelezaji wake umefikia **asilimia 100**;

(ii) Ununuzi wa mabomba umekamilika, na kazi ya ulazaji wa mabomba kwa kilomita **28,** kati ya kilomita **91.9.** Kazi imefikia asilimia **70**,

(iii) Ununuzi wa Mabomba yenye kipenyo cha mm **32** na mm **250**. Upo **asilimia 50**;

(iv) Ujenzi wa Matanki umefikia kwa **asilimia 95.** Kazi zilizobaki ni ufungaji viungio na umaliziaji (finishing).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto ya fedha kuchelewa kutoka kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Ni rai ya Kamati kwamba, fedha zilizotengwa zitolewe kwa wakati na kikamilifu.**

### 2.2.8 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Maji (**Fungu 49**) iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,700,000,000.00**. Hadi mwezi Februari, 2026, makusanyo halisi yalikuwa **Shilingi 850,260,186.00.** Sawa na asilimia **50.2,** ya lengo la mwaka. **Mchanganuo wa**

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli umeainishwa kwenye Kielelezo Na.1**

**Kielelezo Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| MAELEZO | MAPATO YALIYOIDHINISHWA | MAKUSANYO HADI FEBRUARI, 2026 | (%) YA LENGO | SABABU ZA UFANISI |
|---|---|---|---|---|
| Idara ya Utawala na Rasilimali watu | 1,000.00 | 0.00 | 0 | Hakuna Miradi mipya iliyoingiwa mikataba |
| Idara ya Rasilimali Maji | 300,000,000.0 | 22,182,011.00 | 7.39 | Malipo kwa ajili ya leseni kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji |
| Idara ya Huduma za Ubora wa Maji | 1,400,000,000.00 | 828,078,175.00 | 59.15 | Ada kwa huduma za Maabara |
| **JUMLA** | **1,700,001,000.00** | **850,260,186.00** | **50.02** | |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa: -

(a) Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara ya Maji kwa kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa Bajeti **ni asilimia 50.02.** Ya lengo la ukusanyaji kwa mwaka. Ukusanyaji huu uko chini ya kiwango kwa kuwa kipindi hiki unapaswa kuwa zaidi ya **asilimia 66.** Hali hii inahitaji msukumo mkubwa wa Serikali ili lengo la Makusanyo ya Maduhuli lifikiwe ifikapo Juni, 2026;

(b) Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kutokana na Leseni za Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji umefikia **asilimia 7.39.** Kiwango hiki cha Makusanyo si

dalili nzuri kwamba Wizara itaweza kufikia lengo la ukusanyaji wa Maduhuli hayo ifikapo Mwezi Juni, 2026. Vile vile hali hiyo, inaonesha kwamba, upangaji wa lengo haukuzingatia uhalisia;

(c) Mwenendo wa ukusanyaji wa Ada kwa Wateja wanaopata huduma za Maabara za ubora wa maji umefikia **asilimia 59.15.** Mwenendo huu unaashiria huenda lengo la kukusanya lisitimie kama ilivyokusudiwa, mtazamo unaonyesha kuwa, kama huduma za Maabara zitaboreshwa na kusimamiwa ipasavyo, makusanyo ya Maduhuli yanaweza kuongezeka, hivyo kufikia lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika, kwa Uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, uwekezaji wa kutosha katika Leseni za Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji utachangia kuongeza Mapato ya Serikali, na hivyo kuleta tija iliyokusudiwa.**

### 2.2.9 Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha ni hatua muhimu katika utekelezaji wa Bajeti. Aidha, mwenendo wa kiwango cha fedha kinachopatikana kwa mwaka mmoja, ni muhimu katika uamuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa mantiki hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa

fedha kwa Bajeti ya Mwaka 2025/2026, na matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo: -

**(a) Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Fungu 49) lilitengewa jumla ya **Shilingi 73,779,579,000.00.** Kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,081,382,000.00.** Sawa na **asilimia 25** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC), na **Shilingi 55,698,197,000.00.** Sawa na **asilimia 75.0** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Februari, 2026, fedha zilizopokelewa ni jumla ya **Shilingi 8,346,175,604.15.** Kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na **asilimia 46** na **Shilingi 39,130,487,650.00.** Sawa na **asilimia 70** za Mishahara.

**Kielelezo Na. 2: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na Kupokelewa hadi Februari, 2026**

| Fedha iliyoidhinishwa 2025/2026 | | Fedha iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA OC** | **18,081,382,000** | **8,346,175,604.15** | 46.1 |
| **FEDHA ZA MISHAHARA** | **55,698,197,000** | **39,130,487,650.00** | 70.3 |
| **JUMLA** | **73,779,579,000.00** | **47,476,663,254.15** | **64.3** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi katika jedwali unaonesha kwamba utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ambazo zinakusudiwa kutumika katika uendeshaji wa shughuli za uimarishaji wa huduma za Maji Mijini na Vijijini hadi kufikia mwezi Februari 2026, ni **asilimia 64.3.** ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Upatikanaji huo wa fedha ni wakuridhisha ukilinganishwa na kiasi kilichopaswa kufikiwa kwa kipindi hicho**.**

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2026, Fedha zilipokelewa ni kiasi cha **Shilingi 8,346,175,604.15.** Sawa na **asilimia 46.1** kwa Matumizi Mengineyo (OC) ya Bajeti iliyoidhinishwa.


**Mheshimiwa Spika, Mapokezi ya fedha hizo za (OC) hayaridhishi. Ni rai ya Kamati kwamba, Serikali ihakikishe inatoa fedha zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge ifikapo tarehe 30 Juni 2026.**

### 2.2.10 Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha, 2025/26**Fungu 49** liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 824,496,874,000.00.** Kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 340,463,656,000.00.** ni fedha za ndani kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali, na Mfuko wa Taifa wa Maji na **Shilingi 484,033,218,000.00.** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Mwezi Februari, 2026, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 612,384,641,495.19.** Sawa na **asilimia 74.3** ya lengo la fedha za maendeleo. Mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 03**

**Kielelezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo hadi Februari, 2026**




**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Uchambuzi wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo inayolenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ulifikia **asilimia 74.3** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati ni kiashiria kwamba Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa itakamilika kama ilivyokusudiwa ifikapo Juni, 2026;**

(b) Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **aslimia 74.7** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia upatikanaji wa fedha za nje. Aidha, Kamati inasisitiza kuendelea kupunguza utegemezi kwa kutafuta vyanzo vipya vya mapato kwa fedha za ndani, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi.**

(c) Kwa upande wa fedha kutoka nje upatikanaji wake ulifikia **asilimia 73.9** ya Bajeti iliyoidhinidhwa na Bunge. Hali hii inaonesha kwamba mapokeo ya fedha ni ya kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia Upatikanaji wa fedha za Maendeleo. Aidha, inasisitiza kuendelea kupunguza utegemezi kutoka nje na kutafuta vyanzo vipya vya mapato.**

### 2.2.11 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

#### (a) Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Wizara ya Maji

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, ililenga kufanikisha utekelezaji wa Mipango na majukumu ya Wizara ya Maji na Taasisi zake, Katika kufikia malengo ya Kisekta, Kitaifa na Kimataifa. Kamati ilidadisi utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika maeneo Makuu matatu ya Sekta ya Maji. Maeneo hayo ni: -

(i) Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji;

(ii) Huduma ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Vijijini na Mijini;

(iii) Uratibu na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zake;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa shughuli zilizofanyika hadi Mwezi Februari, 2026, ni pamoja na:-

(i) Mradi wa kuboresha huduma ya maji kwa Miji **28** Tanzania Bara, ambapo utekelezaji unaendelea;

(ii) Mtandao wa vituo **1,186** vya kufuatilia mwenendo wa Rasilimali za maji umeanzishwa;

(iii) Vibali 38 vya ujenzi wa Mabwawa ya Topesumu vimetolewa na Mabwawa Saba (7) ya topesumu yamesajiliwa. Vilevile, vibali vitatu (3) vya ujenzi wa Mabwawa ya maji 14 vimetolewa;

(iv) Miti zaidi ya **milioni 6** rafiki wa maji imepandwa, ili kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji, na vibali **247** vya utupaji maji taka vimetolewa ili Kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji;

(v) Ununuzi umefanyika wa vifaa vya uhakiki wa ubora wa maji vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.7.** ; na

(vi) Kuendelea na ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaogharimu **Shilingi 329,466,814,886.00.** ambapo, hadi Mwezi Februari , 2026, ujenzi wa Bwawa hilo umefikia **asilimia 47 ya lengo**;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, zipo changamoto kama zifuatazo:-

**(i) Mahitaji Makubwa ya Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Miradi Mikubwa ya Kimkakati ya Maji.**

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Serikali la Kumtua Mama ndoo Kichwani linahitaji mikakati madhubuti. Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, inaonyesha, Wizara

inakabiliwa na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa rai kwa Serikali, kuendelea na jitihada za dhati, katika kutekeleza ujenzi wa Miradi ya Kimkakati.**

**(ii) Uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji**

**Mheshimiwa Spika,** uelewa mdogo wa Jamii juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na ongezeko la watu, linalosababisha kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi ni vyanzo vikuu vya uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji.

**(iii) Mabadiliko ya tabianchi**

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi yanaathiri nchi yetu, kwa kusababisha mafuriko na ukame wa muda mrefu, hivyo kuchangia kupungua, kukauka na uharibifu kwa vyanzo vya maji na kupungua kwa uzalishaji wa maji.

**(iv) Uendelevu wa miradi ya maji Vijijini**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Serikali katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji Vijijini bado kuna changamoto ya uendelevu wa miradi ya maji katika baadhi ya maeneo. Hali hiyo inachangiwa na

kukauka kwa vyanzo vya maji, wananchi kushindwa kumudu gharama za uendeshaji, matengenezo kutokana na makusanyo hafifu ya mauzo ya maji, na uharibifu wa miundombinu ya maji.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Uchambuzi wa Malengo na Vipaumbele

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji ni msingi wa shughuli zote za maendeleo ya kiuchumi, na kijamii kwa ajili ya usalama wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** malengo na vipaumbele vilivyoainishwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, vinaendana na majukumu ya msingi ya Wizara ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kutekeleza maeneo ya vipaumbele yafuatayo: -

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Miradi **867** ya Maji vijijini, Ujenzi na ukarabati wa Mabwawa 35 na miradi 220 ya maji mijini;

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maji chini ya Mpango wa Mtandao wa Taifa wa Kusambaza Maji, (*National Water Grid)* kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji kama Maziwa na Mito.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Dodoma kupitia Singida, Ziwa Nyasa kwenda mikoa ya Njombe na Ruvuma, Ziwa Tanganyika kwenda mikoa ya Kigoma, Katavi, Songwe na Rukwa;

(iii) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi;

(iv) Kuimarisha uendelevu wa miradi ya maji na ustahimilivu wa sekta dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo kuendeleza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati kama vile Kidunda na Farkwa pamoja na mabwawa madogo ya kati kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua na kuongeza uhakika wa upatikanaji wa maji; na

(v) Kuimarisha ufanisi wa huduma za maji kwa kupunguza upotevu wa maji (*Non-Revenue Water*) kupitia ukarabati wa miundombinu chakavu, kufunga dira za maji za malipo kabla ya matumizi (*prepaid water meters*), pamoja na kuimarisha udhibiti wa wizi wa maji.

## 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

### 3.2.1 Makadirio ya Maduhuli Yatakayokusanywa

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/27, Wizara ya Maji **(Fungu 49**) inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 1,816,109,000.00.** Kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,400,000,000.00.** ni ada za huduma za maabara za maji, **Shilingi 416,108,000.00.** Zinatokana na leseni kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji na vibali vya

matumizi ya maji katika mabonde, na **Shilingi 1,000.** ni mauzo ya nyaraka za zabuni.

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilifanya ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, na Maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa ulinganisho huo unaonekana katika **Kielelezo Na. 04**.

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2025/2026 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2026/2027 | % ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya Nyaraka za Zabuni | 1,000.00 | 1,000.00 | - |
| Leseni za Kampuni za Utafiti | 300,000,000.00 | 416,108,000 | **39** |
| Ada - Huduma za Maabara | 1,400,000,000.00 | 1,400,000,000 | - |
| **JUMLA** | **1,700,001,000.00** | **1,816,109,000** | **7** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya Uchambuzi yanaonesha kuwa: -

(i) Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 limeongezeka, kwa **asilimia 7.** ikilinganishwa na Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa upande wa Leseni za Kampuni za utafiti limeongezeka kwa **asilimia 39**;

(iii) Ada ya Huduma za Maabara haijaongezeka. Uchambuzi huo unaonesha kuwa upangaji wa makadirio umezingatia hali halisi ya utekelezaji wa mwaka wa fedha unaoisha; na

(iv) Makadirio ya makusanyo ya Maduhuli kutokana na Mauzo ya Nyaraka za Zabuni pia haujaongezeka.

**Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kwamba, uzoefu wa makusanyo yaliyopatikana kwa kipindi cha robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 kuwa chini ya kiwango. Serikali iweke mkakati mahsusi wa kuwezesha kukusanya kiasi kilichopangwa kwa wakati.**

### 3.2.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti FUNGU 49

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 1,120,194,614,000.00.** ni ongezeko la **asilimia 25,** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha 2025/2026. Kati ya fedha hizo **Shilingi 80,652,044,000.00.** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 1,039,542,570,000.00.** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo, **Shilingi 401,203,708,946.00.** ni Fedha za Ndani na **Shilingi**

**638,338,862,000.00.** ni fedha za Nje. Uchambuzi wa ulinganisho huo unaonekana katika **Kielelezo Na. 05**.

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| **Na.** | **Maelezo** | | **Bajeti 2025/2026(A)** | **Bajeti 2026/2027(B)** | **TOFAUTI (B-A)** | **% -/+** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | Matumizi ya Kawaida | Mishahara | 55,698,197,000 | 64,378,800,000 | 8,680,603,000 | **15** |
| | | Matumizi mengineyo | 18,081,382,000 | 16,273,244,000 | (1,808,138,000) | **(10)** |
| | **Jumla ndogo** | | **73,779,579,000** | **80,652,044,000** | **6,872,465,000** | **9** |
| **2.** | Matumizi ya Maendeleo | Fedha za Ndani | 340,463,656,000 | 401,203,708,946 | 60,740,052,946 | 18 |
| | | Fedha za Nje | 484,033,218,000 | 638,338,862,000 | 154,305,644,000 | 32 |
| | **Jumla ndogo** | | **824,496,874,000** | **1,039,542,570,000** | **215,045,696,000** | **26** |
| **JUMLA KUU** | | | **898,276,453,000** | **1,120,194,614,000** | **221,918,161,000** | **25** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2026/2027

### 3.2.3 Mchanganuo wa Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Maji **(Fungu 49)** imetengewa jumla ya **Shilingi 80,652,044,000.00.** Kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ongezeko la **asilimia 9.** Ukilinganisha na mwaka unaoisha wa 2025/2026. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,273,244,000.00.** sawa na **asilimia 20.2.** ni kwa ajili ya

kugharamia Matumizi Mengineyo (OC), na **Shilingi 64,378,800,000.00.** sawa na **asilimia 79.8** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. **Mchanganuo wa mgawanyo wa fedha hizo kwa idara na vitengo ni kama unavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 5.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa: -

(a) Bajeti ya Wizara ya kuimarisha huduma ya majisafi na salama imeongezeka kwa **asilimia 9**.

(b) Matumizi Mengineyo (OC) imepungua kwa **Shilingi 1,808,138,000.** sawa na **asilimia 10.**

**Mheshimiwa Spika, Ni rai ya Kamati kuwa, Bajeti hii itatolewa kama ilivyopangwa ili shughuli za usimamizi na uendeshaji wa rasilimali za maji zisimamiwe kwa ukamilifu.**

### 3.2.4 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Maji inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 1,039,542,570,000.00.** kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 401,203,708,000.00**. sawa na **asilimia 39.** ni fedha za ndani na **Shilingi 638,338,862,000.00.** Sawa na **asilimia 61.** ni

fedha za nje. Mchanganuo wake umeonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 5** .

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa:

(a) Bajeti ya Wizara ya Maji kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, imeongezeka kwa **asilimia 26.** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

(b) Bajeti ya fedha za nje imeongezeka kwa **asilimia 32.** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Hali hii ni dalili nzuri kwamba Nchi yetu ina mahusiano mazuri na washirika wa maendeleo. Hata hivyo ni rai ya Kamati kwamba, Serikali ifuatilie kwa karibu ili fedha hizi zitolewe kama zilivyopangwa; na


(c) Serikali itafute vyanzo vipya vya fedha za ndani vyenye uhakika ili kuongeza nguvu katika utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa nyongeza hiyo, Lakini, ni dhahiri kwamba, ongezeko hilo halitoshelezi, ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha zinazohitajika katika kukamilisha utekelezaji wa Mpango mahsusi, wa Taifa wa Kusambaza Maji, (National Water Grid).**

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Kamati imeridhika kwamba Bajeti hii imezingatia azma ya Serikali iliyotamkwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025-2030. Azma hiyo ni kuona kwamba, nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kwamba huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia Wananchi zaidi ya asilimia **85** Vijijini na **95** kwa Mijini ifikapo mwaka 2030.

### 3.2.5 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti ya Serikali

**Kielelezo Na. 6: Ulinganifu wa Jumla ya Bajeti ya Taifa/Serikali dhidi ya Bajeti ya Wizara ya Maji**



**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ili kubaini ongezeko/ pungufu la Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali.

**Mheshmiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Bajeti Kuu ya Serikali ni **Shilingi 62,334,193,000,000.** Wizara ya Maji ni **Shilingi 1,120,194,614,000.00.** sawa na **asilimia 2.** ya Bajeti Kuu ya Serikali. Tathimini inaonyesha Bajeti ya Taifa imeongezeka kwa **asilimia 9.** Wakati Bajeti ya Sekta ya Maji imeongezeka kwa **asilimia 25.** ukilinganisha na Bajeti ya mwaka unaoisha. **Kielelezo Na. 7**: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali 2026/2027.

## 3.3 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.3.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji – **Fungu 49** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naomba kubainisha Maoni ya Kamati ambayo yamezingatia changamoto zinazoikabili Sekta ya maji. Changamoto hizo ni pamoja na: -

(a) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ya maji;

(b) Baadhi ya Taasisi za Serikali kutokulipa deni la Ankara za huduma ya maji, zinazotolewa na Mamlaka za maji;

(c) Taarifa ya Mwaka 2025/2026 ilionyesha changamoto ya malimbikizo ya madeni ya Wakandarasi**,** Washauri elekezi na Wazabuni kuwa ni kiasi cha **Shilingi 534,725,071,524.31.**Hadi Februari 2026, Serikali ilikuwa imelipa **Shilingi bilioni 261.7.** sawa na **asilimia 49** ya deni;

(d) Uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji;

(e) Uelewa mdogo wa Jamii kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji, pamoja na ongezeko la watu linalosababisha kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi;

(f) Upotevu wa maji yanayopotea njiani kutokana na sababu mbalimbali; na

(g) Mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kwa ujumla Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unaridhisha ambao, ni **asilimia 74.3** ya fedha zote za Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, Kamati inaona kuwa, bajeti iliyotengwa haitoshelezi katika kuleta matokeo chanya.

(b) Baadhi ya Taasisi za Serikali kutolipa madeni ya Ankara za maji kwa wakati, kunapunguza uwezo wa Mamlaka za maji kujiendesha;

(c) Madai ya Wakandarasi kutolipwa kwa wakati yanakwamisha utekelezaji wa miradi;

(d) Ushirikiano hafifu kati ya Wizara ya Maji wa kushirikiana na Wizara nyingine, katika kulinda maeneo yanayozunguka vyanzo vya Maji. Mfano wa Taasisi hizo ni Kilimo, Maliasili, Tamisemi, Madini na nyinginezo;

(e) Uchakavu wa Miundombinu na uharibifu wa mabomba, unaosababisha upotevu wa Maji njiani kabla ya kufika kwa Walengwa;

(f) Kukamilika kwa Grid ya Taifa ya Maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika vya maji italeta suluhisho la maji nchini; na

(g) Mabadiliko ya Tabianchi yanayosababisha ukame na kupungua kwa uzalishaji wa maji.

### 3.3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Maoni yaliyobainishwa hapo juu naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:

**(a) Mahitaji Makubwa ya Fedha kwa ajili ya Uwekezaji wa Miradi Mikubwa ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** changamoto kubwa inayoikabili Sekta ya Maji kwa sasa, ni uhitaji mkubwa wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati; changamoto hii inasababishwa na kutegemea fedha za nje ambazo, hazina uhakika kutokana na kubadilika kwa Sera za Kimataifa;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kwamba;

(i) Iendelee kuweka mikakati ya muda mrefu, ambayo itawezesha upatikanaji wa mapato hasa katika kuimarisha vyanzo vya ndani, na kuleta matokeo chanya;

(ii) ili lengo la kumtua mama ndoo kichwani liweze kutimia, Serikali ihakikishe kuwa fedha

zinazoidhinishwa, na Bunge zinatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu;

(iii) Serikali ihimize ujenzi wa miradi mikubwa ya maji kwa njia ya uwekezaji na kuhusisha Sekta binafsi (*PPP)*;

(iv) Serikali iweke kipaumbele katika kukamilisha miradi ambayo tayari imeanza kutekelezwa badala ya kuwa na miradi mingi ambayo haijakamilika. Aidha, kasi iongezeke ya kusambaza maji kwenye maeneo ambayo, miradi ya maji imekamilika;

(v) Maji maji safi na salama yasambazwe kwenye maeneo yanayotoa huduma za kijamii ambayo, miradi ya maji imepita. Maeneo hayo ni kama vile Shule na vituo vya huduma za afya.

**(b) Madeni ya Ankara za Maji kutolipwa kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya baadhi ya Taasisi za Serikali kutokulipa madeni ya Ankara za maji kwa wakati, jambo linalopunguza uwezo wa Mamlaka za maji kujiendesha;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kwamba;

(i) mikakati iwekwe ili Taasisi hizo na wateja binafsi wanaodaiwa Ankara za maji waweze kulipa malimbikizo ya madeni hayo; na

(ii) zifungwe mita janja zinazowezesha kulipa kabla ya matumizi (*prepaid meter*) hususani kwenye Taasisi za Serikali ili kuepusha malimbikizo ya madeni na kudhibiti upotevu wa maji;

**(c) Madai ya Wakandarasi, Washauri Elekezi na Wazabuni**

**Mheshimiwa Spika,** Malimbikizo ya madeni ya Wakandarasi, Washauri elekezi na Wazabuni wa huduma nyinginezo ni changamoto inayoikabili Sekta ya Maji nchini. Hadi kufikia, Februari, 2025, deni hilo lilikuwa limefikia kiasi cha **Shilingi 534,725,071,524.31.** Hadi Februari 2026, Serikali ilikuwa imelipa **shilingi bilioni 261.** sawa na **asilimia 49** ya deni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kwamba, ilipe madai ya wakandarasi kiasi kilichobaki cha **Shilingi bilioni. 273.** Sawa na **asilimia 51.** ili kuepuka kuiongezea Serikali gharama zinazotokana na miradi kutokamilika kwa wakati;

**(d) Uharibifu wa Mazingira Katika Vyanzo vya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayosababisha upungufu wa maji nchini, ni uharibifu wa mazingira, katika vyanzo vya maji, hali inayo sababisha kukauka au kupungua kwa maji katika vyanzo hivyo;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba;

(i) Serikali iweke usimamizi madhubuti katika vyanzo vya maji ikiwemo Mabwawa na Mito kwa mujibu wa sheria pia, kuwe na matumizi sahihi ya maji;

(ii) Katika kudhibiti shughuli zisizokuwa rafiki kwa Mazingira, Wananchi wahimizwe kutunza vyanzo vya maji ili waweze kunufaika na uwepo wa mabwawa na mito kwa muda mrefu zaidi.

(iii) Aidha, Serikali iendelee kuwashirikisha Wananchi kwenye uandaaji na utekelezaji wa miradi ya maji;

(iv) Sekta ya Maji, Mifugo, Kilimo na Uvuvi zishirikiane katika kupanga matumizi ya maji kwenye maeneo ya Mabwawa na mito kwa kuzingatia Miundombinu ya Maji ya kunyweshea Mifugo, shughuli za Kilimo na Uvuvi salama.

**(e) Uharibifu wa Miundombinu, Uchakavu wa Mabomba, Wizi na Upotevu wa Maji Njiani Kabla ya Kufika kwa Walengwa**

**Mheshimiwa Spika,** uharibifu wa miundombinu ya maji, uchakavu wa mabomba na wizi wa maji ni miongoni mwa mambo yanayo sababisha changamoto ya upotevu wa maji njiani kabla ya kufika kwa watumiaji hali inayo sababisha wananchi kukosa huduma licha ya miundombinu kufika kwenye maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba;

(i) Serikali ishirikiane na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi, ili kulinda miundombinu ya maji inayopita maeneo hayo; na

(ii) Serikali iendelee kufanya tathimini na kukarabati mabomba chakavu ili kuepusha upotevu wa maji.

**(f) Mkakati Endelevu wa Kuwa na Grid ya Taifa ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya changamoto inayowakabili Wananchi, ni upungufu wa maji, hasa kipindi cha ukame, kutokana na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya maji vinavyojitosheleza;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba, itenge fedha za kutosha na itoe fedha hizo, ili miradi ya kimkakati, iweze kukamilika kwa kutumia vyanzo vya uhakika vya maji kutoka Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Mto Rufiji na vyanzo vingine.

**(g) Mabadiliko ya Tabianchi**

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi yana athari kubwa kwa jamii; kwani, mvua kubwa iliyonyesha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, imesababisha uharibifu wa Miundombinu ya maji, na maeneo mengine kumekuwa na ukame uliosababisha kupungua kwa uzalishaji wa maji;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba,

(i) Iweke Mikakati mahsusi ya ujenzi wa Mabwawa mengi ya kuvunia maji ya mvua na upandaji miti, kwa lengo la kuhifadhi maji na kudhibiti mafuriko;

(ii) Kuhakikisha kwamba, miundombinu ya maji inayojengwa inakuwa himilivu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;

**(h) Kufunga Dira za Maji za Malipo Kabla ya Matumizi (*Prepaid Water Meters*)**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayoikabili Sekta ya maji, ni watumiaji wa maji kutolipa Ankara za maji kwa wakati. Hali inayosababisha Sekta ya Maji kushindwa kujiendesha ipasavyo kutokana na madeni yasiyolipwa kwa muda mrefu;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali, kuongeza kasi ya kuwaunganisha wateja wake, kwenye dira za maji za malipo kabla ya matumizi, (*prepaid water meters*) ili kupunguza changamoto hiyo**.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi katika Miradi ya Maji. Aidha, Kamati inampongeza Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso na Watendaji wote wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Mwajuma Waziri, kwa kutekeleza Miradi kwa ubora unaolingana na thamani ya fedha iliyotolewa.**

### 3.3.3 Hitimisho

#### (a) Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti. Kamati ya Maji na Mazingira inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema na Maisha marefu. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, hususan wakati wa Uchambuzi wa Bajeti na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Prof. Pius Zebhe Yanda, Mb | - | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb, | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Patali Shida Patali, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Eng. Ramadhani Hamza Singano, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dr. George Venance Lugomela, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Haiderali Hussein Gulamali, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Azza Hillal Hamad, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Thomas Maganga Kampala, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Martha Festo Mariki | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Dickson Lutevele Villa, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Asya Sharifu Omar, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Patrick Adkin Mwalunenge, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Jamal Ramadhan Mwinyi, Mb | - | Mjumbe |

17. Mhe. Mecktridis Fratern Mdaku, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Sanya Jussa Jafari, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na

kumshukuru Waziri wa Maji Mheshimiwa **Jumaa Aweso,** (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa **Mhandisi Kundo Mathew** (Mb), Katibu Mkuu **Mhandisi Mwajuma Waziri,** Naibu Katibu Mkuu **Ndugu Rose Zacharia Ambrose** pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge **Ndugu Baraka Leonard,** kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama.

**(b) Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji **Fungu 49** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.



Jackson G. Kiswaga, Mb,
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA.**

05 Mei, 2026.